HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA KAGERA MEJA JENERALI (MST) SALUM M. KIJUU WAKATI WA UZINDUZI WA BODI YA NNE YA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA KAGERA, TAREHE 17 AGOSTI, 2017

Ndugu Katibu Tawala wa Mkoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Bukoba,

Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri,

Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri,

Ndugu Mwenyekiti wa Bodi na Wajumbe wa Bodi,

Ndugu Wajumbe wa Bodi iliyomaliza muda wake,

Ndugu Waandishi wa Habari,

Washiriki wote,

Mabibi na Mabwana.

Kagera! Kazi, Amani na Maendeleo.
Kazi, Amani na Maendeleo! Kagera.

Ndugu Mwenyekiti,
Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwenye tukio muhimu la uzinduzi wa Bodi ya Ushauri ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

Aidha, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi iliyomaliza muda wake. Asanteni sana kwa kazi kubwa mliyoifanya. Tunajivunia mafanikio yaliyotokana na ubunifu wenu na kujitoa kwenu kuwatumikia Wananchi. Msingi wa

utendaji mliouweka utakuwa mwanzo mzuri kwa Bodi mpya. Kulingana na miongozo, muda wa kuwatumikia wananchi kupitia Bodi umekwisha, ila pale tutakapo hitaji msaada wenu wa mawazo na ushauri msisite kutusaidia.

Ndugu Mwenyekiti,
Kwa namna ya pekee, ninawapongezeni wajumbe wa Bodi mpya kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto na kuwateua kuwa wajumbe wa Bodi. Kwa namna ya pekee, ninampogeza Mwenyekiti wa Bodi kwa kuaminiwa na Wajumbe na kupewa nafasi hii ya kuongoza Bodi hii. Hongereni sana. Ni matumaini yangu kuwa mtaitumikia nafasi hii kwa kiwango cha juu.

Ndugu Mwenyekiti,
Ninaomba kuwakaribisheni sana katika Hospitali yetu hii ya Mkoa ili tushirikiane kuboresha huduma. Tunawategemea sana na tuna imani kubwa na ninyi. Nimetaarifiwa kuwa tayari mmepata mafunzo juu ya majukumu yenu. Pia nimetaarifiwa kuwa wakati wa mafunzo hayo mliweza kupitishwa kwenye baadhi ya changamoto zinazoikabili Hospitali yetu zikiwemo:

1. Upungufu wa watumishi kwa asilimia 53.5% hasa kada ya Madaktari na Madaktari Bingwa.

2. Upungufu wa fedha.

3. Ukosefu wa nyumba za watumishi.

4. Uchakavu wa miundombinu ya Hospitali inayotokana na ukongwe wa Hospitali.

5. Upungufu wa baadhi ya Dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Ndugu Mwenyekiti,
Changamoto hizi zinapelekea utoaji wa huduma kuwa chini ya matarajio lakini jitihada mbalimbali zinaendelea kufanyika ili kukabiliana na changamoto hizi. Ni imani yangu kuwa uwepo wenu ni fursa nyingine ya kuongeza kasi ya kutatua changamoto hizi.

Ndugu Mwenyekiti,
Jitihada zinazoendelea kufanyika ni pamoja na:

i. Kuajiri kwa mkataba madaktari 5 ambao mpaka sasa wanalipwa kutoka fedha za uchangiaji Huduma (Cost sharing). Hata hivyo jitihada zaidi zinahitajika kuhakikisha Madaktari hawa wanapata ajira rasmi na kutafuta Madaktari na watumishi wengine zaidi.

ii. Kwa upande wa nyumba za watumishi, tayari tumepata kiwanja Manispaa ya Bukoba kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi. Mpango uliopo ni kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kulipia kiwanja hicho na kuanza ujenzi kwa awamu.

iii. Kwa upande wa Miundombinu, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ilifanyiwa ukarabati mkubwa kati ya mwaka 1997 hadi 2000 na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na shirika la DANIDA. Hivyo, ni muda mrefu umepita tangu ukarabati huu ufanyike.

    Mpango uliopo ni kufanya harambee kubwa ili kupata fedha za kukarabati na kupanua baadhi ya majengo na miundombinu iliyochoka kama kujenga ***“theatre”*** ya akina mama wajawazito, kujenga chumba cha watoto wachanga chini ya mwezi mmoja (Neonatal Unit), kuboresha

barabara za ndani na kuboresha chumba cha kuhifadhia maiti.

iv. Kuhusu upungufu wa Dawa, kumefanyika jitihada mbalimbali ili kuboresha upatikanaji wa Dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Eneo la kwanza kufanyiwa kazi na Serikali ni kuongeza bajeti ya fedha za kununulia dawa katika Hospitali hii kutoka shilingi milioni 143 mwaka 2015/16 hadi milioni 518 kwa mwaka 2016/17. Ongezeko hilo limeleta mabadiliko makubwa katika upatikanaji wa dawa ndani ya Hospitali yetu.

    Shauku yangu ni kuwa na upatikanaji wa dawa kwa asilimia 100. Ili kufanikisha hili, tumeanzisha Duka la Dawa ambalo tutalizindua leo.
    Ndugu Mwenyekiti, tushirikiane kusimamia ili Duka hili lifanyekazi na kukidhi matarajio ya wananchi.

v. Ili kuongeza mapato na kuongeza ubora wa takwimu, umefungwa mfumo wa Kielektroniki katika baadhi ya maeneo ya Hospitali. Mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha makusanyo yote yanafanyika kwa njia ya Kielektroniki. Changamoto ni kupata kompyuta zaidi ya 40 ili kuhakikisha kuwa mfumo unasambaa katika Hospitali nzima.

Ndugu Mwenyekiti,
Haya ni baadhi tu ya maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa maboresho. Bodi ikianza kazi na kupata taarifa za kina juu ya Hospitali hii, mtaweza kuibua mambo mengine ambayo yanatakiwa kuboreshwa zaidi.

Ndugu Mwenyekiti,
Ofisi yangu iko tayari kushirikiana na Bodi katika kutatua changamoto hizi. Tukiunganisha nguvu kwa pamoja na kwa kushauriana, kubuni na kutekeleza kwa pamoja hakika mambo haya yataboreka na hatimaye kuboresha huduma kwa wananchi. Narudia kusema tunawategemea sana, na tuna imani kubwa kwenu.

Baada ya hayo, ninawashukuru tena na sasa ninatamka rasmi kuwa Bodi ya Nne ya Ushauri ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera imezinduliwa rasmi.

Kagera! Kazi, Amani na Maendeleo.
Kazi, Amani na Maendeleo! Kagera.

Asanteni kwa kunisikiliza.